**OWM-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO**

Shule ya Sekondari Lugoba,
**S.L.P. 81,**
**CHALINZE.**

**Kumb.Na. LSS/F.I – 2015** Tarehe 15/12/2014

MWANAFUNZI----------------------------------.

SHULE YA MSINGI…………………………..

NDUGU,

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2015**

(1) Kichwa cha habari hapo juu chahusika.

(2) Kwa barua hii nakujulisha kuwa umechaguliwa kuingia Kidato cha **kwanza mwaka 2015**, Shule ya Sekondari Lugoba. Unatakiwa kufika shuleni bila kukosa tarehe **04/01/2015** na ufike kabla ya saa kumi jioni.

(3) Shule hii ipo Mkoa wa Pwani katika wilaya ya Bagamoyo. Ipo umbali wa kilometa kama 20 kutoka mji wa Chalinze barabara kuu kuelekea Arusha/Tanga.

(4) Kwa wanafunzi wenye matatizo ya kiafya walete cheti cha kupimwa Afya kutoka hospitali ya serikali.

Mkuu wa Shule na wafanyakazi wote wa Shule hii wanakupongeza na wanakutarajia uwe mwanafunzi MTIIFU, NADHIFU, MWAMINIFU na Mshiriki wa kazi zote za nje na darasani.

**KARIBU SHULE YA SEKONDARI LUGOBA**

**………………………………………**
**ABDALLAH SAKASA**

**MKUU WA SHULE**

**UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI LUGOBA**

**SEHEMU A (Ijazwe na Mwanafunzi).**

Mimi (Jina Kamili ) -----------------------------------------------------------
Nilizaliwa tarehe ----------------- mwezi ------------ mwaka -----------------------
Dini ---------------------------------Katika Kijiji cha -------------------- ---------
wilaya ------------------------------------------

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Lugoba. Nathibitisha kuwa nitatii na kuzifuata sheria zote za Shule ambazo mwanafunzi analazimika kutekeleza na kutimiza.Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiriki katika migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa Shule ili uweze kutatua au kutafutia utatuzi wa changamoto zozote zitakazojitokeza Shuleni.

Saini ---------------------------------------------------------

**SEHEMU B: (Ijazwe na mzazi)**

Mimi (Jina kamili) -------------------------------------------------------
wa Kijiji cha ------------------------------- wilaya ya -----------------------------
Dini---------------------------------------- Kazi-------------------------------------

Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mtoto wangu. Nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule. Pia nitahakikisha mtoto anaenda Shule muda uliopangwa na nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na Shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.

Saini ya Mzazi -----------------------------------------------------

Jina la Mwenyekiti wa kijiji au Afisa mtendaji wa kijiji

---------------------------------------------------------------------

Saini ya Mwenyekiti wa kijiji au Afisa Mtendaji wa Kijiji

……………………………………………………………………….

**SARE ZA SHULE**

Shuleni unalazimika kununua t shirt za njano tu kwa gharama ya shilingi 16,000 tu kwa t shirt 2 UTALIPA OFISINI WAKATI WA KURIPOTI

**MSICHANA**

1.Sketi rangi kijani iliyoshonwa linda ya V mbele isiwe na mpasuo, aje na sketi 2 au zaidi.
2. Shati mikono mifupi (TOMATO) aje na mashati mawili au zaidi.
3. Viatu rangi nyeusi vya ngozi vinavyopigwa kiwi na kufungwa kwa gidamu **usimnunulie bajaji.**
4. Soksi rangi nyeupe
5. Sketi rangi dark blue iliyoshonwa linda ya V mbele isiwe na mpasuo, aje na sketi 2 au zaidi.
6. T shirt nyeupe isiyo na maandishi wala picha, aje na mbili au zaidi.
7. Aje na khanga au kitenge doti moja, taulo na nguo za kulalia.

**MVULANA**

1.Suruali rangi nyeusi iliyoshonwa linda 2 mbele kila upande, aje na suruali 2 au zaidi.
2. Shati mikono mifupi (TOMATO) aje na mashati mawili au zaidi.
3. Viatu rangi nyeusi vya ngozi vinavyopigwa kiwi na kufungwa kwa gidamu
4. Soksi rangi nyeusi
5. Suruali rangi dark blue iliyoshonwa linda 2 mbele kila upande, aje na suruali 2 au zaidi.
6. T shirt nyeupe isiyo na maandishi wala picha, aje na mbili au zaidi.
7. Aje na taulo na nguo za kulalia.

**Wanafunzi Waislam Wasichana**.

Wanaruhusiwa kuvaa sketi ndefu kijani, nusu kanzu nyeupe kitambaa cha tetron usishone kitambaa aina ya sukari na HIJAB nyeupe inayofunika kifua chote

**NB**: Sweta za Shule ni za rangi ya kijani kwa watakaohitaji wanaweza kununua shuleni gharama ni shilingi 15,000/= kwa moja UTANUNUA SHULENI

**Nguo za nyumbani na Simu haziruhusiwi**
**Kuvaa Suruali za kubana na mlegezo ni kosa LITAKALOMFUKUZISHA mwanao SHULE**

**ADA NA MICHANGO MINGINE KWA MUHULA WA KWANZA JANUARI HADI JUNI 2015**

| | |
|---|---|
| Ada Januari hadi Juni 2015 Tshs. | 10,000/= |
| Mchango wa chakula Januari hadi Juni Tshs. | 100,000/= |
| Mchango wa Taaluma Januari hadi Juni Tshs. | 5,000/= |
| Mchango wa Hosteli Januari hadi Juni Tshs. | 7,500/= |
| Mchango wa Matibabu Januari hadi Juni Tshs. | 5,000/= |
| Kitambulisho ni Tshs -------------------------- | 5,000/= |
| Ukarabati wa madawati.----------------- | 5,000/= |
| Kuchangia uboreshaji wa Maabara……………… | 10,000/= |
| Tahadhali………………………………………. | 5,000/= |
| Ukarabati wa majengo na samani……………… | 10,000/= |
| Mchango wa maji na umeme kwa muhula…….. | 5,000/= |
| Mahafali ya kidato cha sita 2015 | 2,500 |
| **JUMLA NI TSHS.** | **170,000/=** |

**Unapaswa kulipia Benki yoyote ya NMB akaunti namba 21101100003 LUGOBA SECONDARY SCHOOL . Na kisha wasilisha nakala halisi ya benki (Bank Pay in Slip) MTOTO HATAPOKELEWA BILA MALIPO KUKAMILIKA**

**KWELI KUSOMESHA NI GHARI LAKINI UJINGA NI GHARAMA ZAIDI. KARATASI ZA MALIPO ZINAPOKELEWA OFISINI KWA MKUU WA SHULE KUANZIA TAREHE 27/12/2014**

**VIFAA VINGINE**

1. Alete picha 3 pasport size,
2. mkebe wa vifaa vya hesabu,
3. madaftari 11 makubwa na
4. Rim moja **A 4 ZA PHOTOCOPY** atakayoikabidhi ofisini.
5. Fagio la chelewa lenye mpini,
6. Ndoo ndogo ya plastic,
7. Sahani, kijiko na kikombe,
8. Slesher,panga na jembe lenye mpini
9. Shuka 2 za rangi yoyote
10. CHANDARUA utapata shuleni ukiwahi kuripoti

**KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARI LUGOBA**